


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO
BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI



TAARIFA KWA UMMA
USAJILI WA MITIHANI YA 25 YA BODI

Dar es salaam 25 Julai, 2022

Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) inapenda kuwajulisha wadau wake kuwa, mitihani ya 25 ya Bodi inatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe **22/11/2022 mpaka tarehe 25/11/2022**. Watahiniwa wote wanaelekezwa kufanya usajili kwa kupitia <https://registration.psptb.go.tz> na kuhudhuria madarasa ya mafunzo kama sehemu ya maandalizi ya mitihani hiyo. Mwisho wa kupokea maombi ya mitihani ya 25 ya Bodi ni tarehe **26/10/2022**.

WAOMBAJI WENYE SIFA KWA AJILI YA MITIHANI YA NOVEMBA, 2022:

- (1) Wahitimu wote waliomaliza vyo vya Elimu ya Juu na Kati kwa ngazi za shahada, stashahada na astashahada ya Ununuzi na Ugavi kwa kipindi cha kuanzia 2022 kurudi nyuma ambao hawakuwahi kufanya mitihani ya kitaaluma ya Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi.
- (2) Wafanyakazi wote wanaofanya kazi za Ununuzi na Ugavi wasiokuwa na cheti cha CPSP.
- (3) Wahitimu wenye taaluma nyingine nje ya ununuzi na ugavi kwa ngazi za stashahada, shahada au sifa za kitaaluma kutoka Bodi ya taaluma husika.

NB. Watahiniwa wanaorudia mtihani zaidi ya ngazi moja wanaruhusiwa kuunganisha ngazi mbili zinazofuatana kwa masomo kuanzia mawili hadi Sita tu.

Kwa maelekezo au ufafanuzi zaidi tafadhali piga simu namba **0738441972** au tuma barua pepe kupitia **examinations@psptb.go.tz**

Imetolewa na

Godfred B. Mbanyi
MKURUGENZI MTENDAJI

